


Kwa nini uchanjwe?



Chanjo ya COVID-19 ni salama na inafanya kazi. Ingawa baadhi ya watu bado wanaweza kuambukizwa COVID 19 baada ya kuchanjwa, chanjo inakusaidia kuzuia kuugua sana au kutafuta matibabu hospitalini ukiambukizwa COVID-19.

Kuchanjwa hupunguza hatari ya kuambukizwa au kuwasambazia watu wengine virusi hivi. Hii ni muhimu katika kuwalinda watu ambao bado hawawezi kuchanjwa, kama vile watoto wadogo.



Pia husaidia kuhakikisha kuwa hospitali zina vitanda vya kutosha kwa watu wote na wale ambao wanahitaji huduma ya dharura wanaweza kuipata haraka.